# Mpango wa Usaidizi wa Kupanga Nyumba wa Dharura (ERAP)
# Maagizo ya Kutuma Ombi na Orodha ya Ukaguzi

Ili familia istahiki, ni lazima ilipe kodi ya makazi ya kuishi na:

1. Mwanafamilia anapaswa kuwa mkaazi wa Kaunti ya Ada, Idaho; na
2. Mwanafamilia anapaswa kuwa na mapato YASIYOZIDI 80% ya Mapato ya Kati ya Eneo; na

| Idadi ya Wanafamilia | Mtu 1 | Watu 2 | Watu 3 | Watu 4 | Watu 5 | Watu 6 | Watu 7 | Watu 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiasi cha Mapato (80% AMI) | $42,200 | $48,200 | $54,250 | $60,250 | $65,100 | $69,900 | $74,750 | $79,550 |

3. Mtu mmoja au zaidi walio katika familia wamestahiki kwa manufaa ya kutokuwa na ajira; **AU** mapato ya mwanafamilia yamepungua, amekuwa na gharama kubwa, au amekuwa na shida nyingine za pesa kwa sababu ya mkurupuko wa COVID 19 moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja; na
4. Mtu mmoja au watu wawili walio katika familia wako hatarini mwa kutokuwa na makao au wana changamoto za kuwa na makao.

## Orodha ya kukagulia Hati:

- ☐ Ombi la Mpango lenye maswali yaliyokamilishwa
- ☐ Idhini ya Kutoa Taarifa
- ☐ Uandikishaji wa Mapato (toa hati zote zinazohusika):

| | |
|---|---|
| Kutokuwa na ajira | Nakala ya ilani ya manufaa au chapisho la malipo uliyopata kwa miezi miwili iliyopita |
| Mapato ya Ajira | Malipo ya ushuru ya 2020, W2; **AU** karatasi ya mshahara na makato yake ya miezi miwili iliyopita |
| Kujiajiri | Malipo ya ushuru ya 2020, 1099, ripoti ya faida na hasara kutoka kwenye mfumo wa uhasibu wa mwombaji, au stetimenti za benki kwa miezi miwili iliyopita |
| Manufaa ya Usalama wa Kijamii | Maelezo ya ushuru ya 2020 au nakala ya barua ya sasa ya tuzo |
| Matunzo ya Watoto | Chapisho la malipo uliyopokea kwa miezi miwili iliyopita, uthibitisho ulioandikwa kutoka kwa mzazi ambaye hayupo, au stetimenti za benki za miezi miwili iliyopita |
| Mapato Mengine | Hati kutoka kwa chanzo zinazoelezea kiwango cha kila mwezi kilichopokelewa. Kwa mfano, pensheni ya VA, malipo ya mwaka, mapato ya ulemavu, fidia ya wafanyikazi, masurufu, nk.) |

- ☐ Kodi na Usaidizi wa Huduma: Huduma zinajumuisha umeme, gesi, maji, majitaka, takataka, intaneti, na gharama za nguvu, kama vile petroli. Huduma za mawasiliano za simu (simu, kebo) hazichukuliwa kama huduma.

  - Mkataba wa sasa wa Kukodisha (kurasa zote)
  - Nakala ya ilani ya kosa la kodi (ikiwa inahusika)
  - Taarifa ya mawasiliano ya mwenye nyumba
  - Bili ya huduma ya hivi karibuni sana (ikiwa unaomba usaidizi wa huduma)

Tafadhali jua kwamba unaweza kuambiwa uwasilishe hati nyingine. Kiwango cha juu zaidi cha usaidizi ambacho wanafamilia wanaweza kupata kinategemea mahitaji na upatikanaji wa fedha. Rudisha ombi lilokamilishwa na hati zote muhimu kwa barua pepe kwenye erap@bcacha.org, faksi (208) 345-4909, au utume barua kwa Boise City/Ada County Housing Authorities Attn: ERAP 1001 S. Orchard St. Boise, ID 83705.

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

BOISE CITY/ADA COUNTY HOUSING Authorities

# Ombi la Mpango wa Usaidizi wa Kodi wa Dharura na Fomu ya Kujiandikisha

## Sehemu ya 1: Taarifa ya Msingi ya Mwombaji

Jina la Mwisho: ______________________ Jina la Kwanza: ______________________ MI: ________

Anwani: ______________________________ Jiji: ____________ Jimbo: ______ Msimbo wa Posta: ____________

Nambari ya Simu ya Nyumbani: ________________ Nambari ya Simu ya Mkononi: ______________________

Barua pepe: ________________ Tarehe ya Kuzaliwa: ____/____/______ Jinsia: ______ Lugha Unayopendelea: ________

Mbari: ☐ Mzungu ☐ Mmarekani mwenyi asili ya Kiafrika ☐ Mwasia ☐ Mhindi wa Marekani /Mwenyeji wa Alaska ☐ Mhawai Asili/ Mkazi wa kisiwa cha Pasifiki

Mhispania au Mlatino? ☐ Ndiyo ☐ Hapana Idadi ya Wanafamilia: _____ (*Watu wazima:* ________ *Watoto:* ________)

Majina ya wanafamilia wote ambao ni watu wazima: ______________________________________

Majina ya wanafamilia wote wenye umri wa chini ya miaka kumi na nane: ______________________________

## Sehemu ya 2: Matatizo ya Kifedha ya COVID-19 Tafadhali tia alama kwenye ZOTE zinazohusika:

- ☐ Kutokuwa na ajira kwa siku 90 kabla ya ombi hili;
- ☐ Ulipoteza mapato sana kwa sababu ya COVID-19;
- ☐ Kupoteza kazi;
- ☐ Fidia Ilipunguzwa;
- ☐ Mahali pa kazi palifungwa;
- ☐ Wajibu wa kutoenda kazini ili umtunze mtoto mwenye umri wa kwenda shuleni aliye nyumbani;
- ☐ Ulipata gharama kubwa ya kimatibabu kwa sababu ya COVID-19.
- ☐ Unahitaji kukaa kwenye karantini kwa sababu ya utambuzi wa COVID-19.
- ☐ Unahitaji kukaa kwenye karantini kulingana na ushauri wa mhudumu wa afya, au ushauri au maagizo ya mamlaka ya afya ya umma ya serikali za eneo lako au jimbo, agizo la afisa wa utekelezaji wa sheria, au una sababu ya kuamini kwamba kukaa kwenye karantini ni bora zaidi kwa afya ya umma na usalama wa binadamu kwa sababu ya uwezo wa kuambukizwa au shughuli za hatari.
- ☐ Hali nyingine inayohusika: ________________

## Sehemu ya 3: Hali ya Nyumba (tia alama kwenye zote zinazohusika)

***Hati Inayohitajika:*** *Ambatisha nakala ya mkataba wako wa sasa wa kukodisha na/au bili ya huduma ya hivi karibuni sana (ikiwa inahusika).*

- ☐ Hatarini mwa kukosa makao au kuwa na changamoto za kuwa na makao kwa sababu ya kukosa kulipa *deni* ya kodi na / au ya huduma
  - Kiwango cha deni ya kodi: ______________________________
  - Kiwango cha deni ya huduma: ____________________________
- ☐ Hatarini mwa kukosa makao au kuwa na changamoto za kuwa na makao kwa sababu ya kutoweza kulipa kodi za *siku zijazo*
  - Kiwango cha deni: ________________ Tarehe ya kulipa: ____________

Je, unaishi kwenye nyumba ya serikali? ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Ikiwa jibu ni ndiyo, Tafadhali taja mpango/mali: ______________________________________

Je unapokea usadizi wowote wa kodi/huduma kwa sasa? ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Ikiwa jibu ni ndiyo, Tafadhali taja mpango/shirika: ______________________________________

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

Je, umetuma ombi la usaidizi wa kodi/huduma kutoka kwenye shirika ligine? ☐ Ndiyo ☐ Hapana

Ikiwa jibu ni ndiyo, Tafadhali taja mpango/shirika: ______________________________

Jina la Mwenye nyumba: ______________________________

Anwani: ____________________ Jiji: __________ Jimbo: ________ Msimbo wa Posta: ______

Nambari ya Simu ya Mwenye nyumba: ________________Barua pepe ya Mwenye nyumba: __________

## Sehemu ya 4: Mapato ya Wanafamilia

***Hati Inayohitajika:*** *Ambatisha nakala za W2 za 2020, malipo ya ushuru, 1099, AU karatasi za mshahara na makato yake ya miezi miwili iliyopita ya watu wote wazima, stetimenti za malipo ya pensheni, barua ya(za) tuzo za usalama wa kijamii, barua ya(za) kutokuwa na ajira, na/au hati ya mapato mengine yoyote ya familia.*

Kwenye chati ifuatayo, tafadhali orodhesha JUMLA ya malipo ya kila mwezi (kabla ya ushuru) ya wanafamilia **WOTE**.

| Jina la Mwanafamilia | Ajira au Mshahara | Mapato ya Kujiajiri na ya Biashara | Pensheni/ Mapato ya Kustaafu | Usalama wa Kijamii, Kustaafu, Ulemavu | TANF ya Kutokuwa na ajira, Usaidizi mwingine wa Umma | Matunzo ya Watoto, Masurufu, Malipo ya Malezi | Mapato Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Jumla** | | | | | | | |
| | | | | | **Jumla ya Mapato ya kila Mwezi:** | | |
| Wanafamilia wafuatao hawana **mapato yoyote**: | | | | | | | |

**Idadi ya Wanafamilia: ______Jumla ya Mapato ya Wanafamilia kutoka katika Vyanzo vyote (Jumla ya Mapato ya Kila mwezi x 12):** ____________

***(Tafuta idadi ya wanafamilia wako kisha uangalie pande nyingine na utie alama kwenye kiwango kinachofaa cha mapato ya kila mwaka)***

| Idadi ya Wanafamilia | 0-30% Mapato ya Chini Kabisa | ✓ | 30%-50% Mapato ya Chini Sana | ✓ | (50%-80%) Mapato ya Chini | ✓ | (Zaidi ya 80%) Zaidi ya | *Haistahiki* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtu 1 | 0 mpaka $15,850 | | Mpaka $26,400 | | Mpaka $42,200 | | Zaidi ya $42,200 | *Haistahiki* |
| Watu 2 | 0 mpaka $18,100 | | Mpaka $30,150 | | Mpaka $48,200 | | Zaidi ya $48,200 | *Haistahiki* |
| Watu 3 | 0 mpaka $21,960 | | Mpaka $33,900 | | Mpaka $54,250 | | Zaidi ya $54,250 | *Haistahiki* |
| Watu 4 | 0 mpaka $26,500 | | Mpaka $37,650 | | Mpaka $60,250 | | Zaidi ya $60,250 | *Haistahiki* |
| Watu 5 | 0 mpaka $31,040 | | Mpaka $40,700 | | Mpaka $65,100 | | Zaidi ya $65,100 | *Haistahiki* |
| Watu 6 | 0 mpaka $35,580 | | Mpaka $43,700 | | Mpaka $69,900 | | Zaidi ya $69,900 | *Haistahiki* |
| Watu 7 | 0 mpaka $40,120 | | Mpaka $46,700 | | Mpaka $74,750 | | Zaidi ya $74,750 | *Haistahiki* |
| Watu 8 | 0 mpaka $44,660 | | Mpaka $49,700 | | Mpaka $79,550 | | Zaidi ya $79,550 | *Haistahiki* |

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

## Sehemu ya 5: Uthibitisho na Udhibitisho wa Ustahiki

Mimi______________________________________, ninasema kwamba nyumba yangu ina angalau mtu mmoja au zaidi ya mmoja anayelazimika kulipa kodi kwenye makao ya makazi na yuko hatarini mwa kukosa makao au kuwa na changamoto za kuwa na makao, na kwa hiyo anatimiza kigezo cha kustahiki kwa hali ya makazi ya mapato ya chini ya 80% ya AMI (Mapato ya Kati ya Eneo). Familia yangu inaweza kuonyesha hatari hii ya kukosa makazi au changamoto za kuwa na makao kwa kutoa hati zinazohitajika kama inavyotakiwa katika ombi hili au kuthibitisha kutokuwa na uwezo wa kulipa kodi au huduma.

Isitoshe, mwanafamilia wangu ana shida ya kifedha inayohusiana na COVID 19, ikiwa ni pamoja na:

1. Anastahiki kwa manufaa ya kutokuwa na ajira; AU

2. Mapato ya familia yalipungua, alikuwa na gharama kubwa, au alikuwa na shida nyingine za kifedha kutokana na ugonjwa wa virusi vya korona (COVID-19).

**<u>KUCHUKULIWA HATUA KWA AJILI YA TAARIFA YA UONGO</u>**

**ONYO: SEHEMU YA 1001 YA HAKI YA 18 YA KANUNI YA MAREKANI INASEMA KWAMBA KUTOA TAARIFA ZA UONGO KWA MAKUSUDI AU KUPOTOSHA IDARA YOYOTE AU SHIRIKA LA MAREKANI KUHUSU SUALA LOLOTE NDANI YA MAMLAKA YAKE NI KOSA LA JINAI. NINAELEWA KWAMBA NIKITOA TAARIFA YA UONGO, ISIYO KAMILI AU ISIYO SAHIHI IKIWA NINAJUA NITAADHIBIWA CHINI YA SHERIA ZA SERIKALI AU JIMBO NA HUENDA NIFUNGULIWE MASHTAKA NA NILIPE TENA USAIDIZI.**

NIMESOMA YALIYO HAPA JUU NA NINAELEWA MAJUKUMU YANGU. NINADHIBITISHA KWAMBA TAARIFA NILIYOPEANA NI SAHIHI NA KAMILI KAMA NINAVYOJUA. NINADHIBITISHA KWAMBA BADO SIJAPEWA USAIDIZI WA KODI AU HUDUMA, KUPITIA MPANGO MWINGINE WOWOTE, INAYOGHARAMIA GHARAMA ZINAZOHITAJIKA KWENYE OMBI HILI.

KWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHA FOMU HII NINAKUBALI KWAMBA JINA LANGU LILILOANDIKWA LITATUMIKA KISHERIA KAMA SAINI ILIYOANDIKWA KWA MKONO KADRI INAVYORUHUSIWA NA SHERIA INAYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| ______________________________ | ______________________ |
| Saini ya Mwombaji wa Msingi | Tarehe |

Ni sera ya BCACHA kuhakikisha kwamba kila mtu bila kujali mbari, dini, rangi, jinsia, umri, nchi asilia, hali ya kifamilia, utambulisho wa kijinsia, hisia za mapenzi, au ulemavu atakuwa na nafasi sawa katika kupata nyumba za bei rahisi. Ikiwa wewe au mtu yeyote aliye katika familia yako ni mtu mwenye ulemavu, na unahitaji makazi maalum ili utumie mpango wetu na huduma zetu kikamilifu, tafadhali wasilisha ombi kwa maandishi au uwasiliane na ofisi yetu kwa (208) 363-9710.

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY